

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 46 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) DISEMBA 2024

KAMATIYA BUNGE YATEMBELEA MRADI WA UJEZI WA OFISI ZA TSC, YATOA MAELEKEZO

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya TAMISEMI, Mhe. Justin Lazaro Nyamoga (Mb) (wa pili kushoto) akiongoza wajumbe wa Kamati hiyo walipotembelea mradi wa ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Makao Makuu unaojengwa Njedengwa jijini Dodoma tarehe 5 Novemba, 2024.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania



[tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

KONGOLE TSC KWA KUANZA MCHAKATO WA KUANDAA MWONGOZO WA MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WANAIAJIRIWA KWENYE UTUMISHI WA UMMA

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeanza mchakato wa kuandaa Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaoajiriwa kwenye Utumishi wa Umma ili waweze kuzingatia masuala muhimu yanayohusu Utumishi wao.

Mwongozo huo unaandaliwa ili kuondoa utofauti katika kuwaelekeza walimu wapya mara wanapoajiriwa kwa kuwa kwa sasa hakuna mwongozo mahususi unaowezesha Ofisi za TSC ngazi ya wilaya kutoa elimu kwa walimu wapya kazini.

Mwongozo umetoa maelekezo mahususi kwa Walimu wapya kuhusu

Misingi ya Utumishi wa Umma na Utumishi wa Walimu, haki na wajibu wao na miiko ya maadili katika utekelezaji wa majukumu yao na taratibu zingine.

Hivyo, tunaipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kuona umuhimu wa kuandaa mwongozo huo ambao kwa kiasi kikubwa utawasaidia walimu wanaoajiriwa katika Utumishi wa Umma Tanzania bara kupata uelewa mzuri wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia Utumishi wa Umma kwa ujumla na hivyo kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia mambo hayo.

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



KAMATI YA BUNGE YATEMBELEA MRADI WA UJEZI WA OFISI ZA TSC, YATOA MAELEKEZO

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Kamati ya Bunge ya Kudumu ya TAMISEMI tarehe 05 Novemba, 2024 ilitembelea mradi wa ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Makao Makuu unaojengwa katika kiwanja na. 77, kitalu BB eneo la uwekezaji Njedengwa jijini Dodoma.

Mradi huo unatekelezwa kupitia Mkandarasi SUMA JKT na umefikia asilimia 50 ambapo hadi kukamilika kwa jengo hilo kiasi cha shilingi bilioni 6.36 zitatumika.

Wajumbe wa Kamati hiyo wakiongozwa na mwenyekiti wake, Mhe. Justin Nyamoga (Mb) walipata fursa ya kukagua maendeleo ya mradi huo na kuonesha kutoridhiswa na kasi ya ujenzi.

Kutokana na hayo Kamati hiyo iliagiza kuwa Ofisi ya Rais TAMISEMI ikae na SUMA JKT ili kutafuta namna bora itakayowezesha mradi huo kukamilika kwa haraka zaidi huku mkandarasi huyo akitakiwa kueleza ni kwa namna gani atakamilisha kazi hiyo kwa wakati.

Pia iliagizwa kuwa, Ofisi ya Rais TAMISEMI ishirikiane na Wizara ya Fedha kuhakikisha fedha za mradi huo zinatolewa kwa wakati ili mkandarasi akamilishe ujenzi kama inavyohitajika.

Vilevile, Kamati hiyo ilielekeza kuwa SUMA JKT izingatie thamani ya fedha kwa kujenga kwa kuzingatia viwango vya ubora unaokubalika ili jengo hilo liweze kudumu muda mrefu huku msimamizi wa mradi (project manager) akitakiwa kuongeza bidii katika usimamizi wa kila hatua ya ujenzi huo.

Awali, akiwasilisha taarifa ya mradi huo kwa upande wa Tume, Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama alieleza kuwa jengo hilo lenye sakafu nne lina



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akitoa neno la utangulizi wakati wa ziara ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya TAMISEMI kwenye mradi wa ujenzi wa Jengo la Ofisi ya TSC Makao Makuu unaojengwa Njedengwa jijini Dodoma iliyofanyika tarehe 5 Novemba, 2024.

eneo la ukubwa wa mita za mraba 3,608 na litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kuchukua watumishi 134.

“Gharama za mradi huu hadi kukamilika ni Shilingi 6,367,329,651.95, fedha iliyolipwa kulingana na kazi iliyofanyika ni shilingi 1,646,685,536.20. Maendeleo ya ujenzi hadi tarehe 05.11.2024 yanakadiriwa kuwa asilimia 50. Muhututari wa kazi zilizofanyika tangu ujenzi ulipoanza ni Upimaji Udongo (Geotechnical Investigation), kazi za awali, kusafisha eneo, kujenga msingi wa jengo, ujenzi wa sakafu ya chini hadi ya pili. Kwa sasa ujenzi umefikia katika hatua ya nguzo za sakafu ya tatu pamoja na ujenzi wa kuta za tofali sakafu ya pili”, alieleza Mwl. Nkwama.

Aliongeza kuwa kazi zilizobaki ili kukamilisha mradi huo ni ujenzi wa nguzo, ujenzi wa *ring beam*, Kupaua na Kuezeka, umaliziaji ujenzi wa kuta za Tofali na Aluminiam, kupiga lipu nje

na ndani, kufunga mifumo ya umeme, maji safi, maji taka, lift na TEHAMA, kutengeneza dari, kuweka marumaru, kuweka madirisha na milango, kuskimu na kupaka rangi, kazi nje ya jengo (maegesho, bustani), kuondoa vifaa site na kukabidhi mradi.

Kwa upande wa taarifa ya Mkandarasi SUMA JKT ilieleza kuwa kazi zinazotarajiwa kuendelea ni kukamilisha kazi za *formwork*, kufunga chuma na kumwaga zege ya sakafu ya tatu (*Third floor slab*) ambazo zilitarajiwa kukamilika kabla ya tarehe 15 Novemba 24.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa ili kukamilisha kazi zote za mradi kama ilivyopangwa ikiwa ni pamoja na kufidia muda uliopotea kutokana na changamoto mbalimbali, Mkandarasi anatarajia kuomba kuongezewa muda wa utendaji kazi, kuongeza idadi ya wafanyakazi ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi pamoja na kuongeza vitendea kazi.

KAMATI YA BUNGE YATEMBELEA MRADI WA UJEZI WA OFISI ZA TSC, YATOA MAELEKEZO



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa Jengo la Ofisi za TSC Makao Makuu wakati wa zaiara ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya TAMISEMI kwenye mradi huo iliyofanyika tarehe 5 Novemba, 2024.



Major S. S. Jambo kutoka SUMA JKT akiwasilisha taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa Jengo la Ofisi za TSC Makao Makuu wakati wa zaiara ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya TAMISEMI kwenye mradi huo iliyofanyika tarehe 5 Novemba, 2024.



Meneja mradi wa ujenzi wa Jengo la Ofisi za TSC Makao Makuu, Mhandisi Arrif Almas akitoa maelezo ya mradi wakati wa zaiara ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya TAMISEMI kwenye mradi huo iliyofanyika tarehe 5 Novemba, 2024.



Mjumbe wa kamati ya Bunge ya Kudumu ya TAMISEMI, Mhe. Godwin Kunambi (Mb) akitoa mchango wake wakati wa zaiara ya Kamati ya Bunge hiyo kwenye mradi wa ujenzi wa Jengo la Ofisi za TSC Makao Makuu iliyofanyika tarehe 5 Novemba, 2024.



Mjumbe wa kamati ya Bunge ya Kudumu ya TAMISEMI, Mhe. Magreth Sitta (Mb) akitoa mchango wake wakati wa zaiara ya Kamati ya Bunge hiyo kwenye mradi wa ujenzi wa Jengo la Ofisi za TSC Makao Makuu iliyofanyika tarehe 5 Novemba, 2024.

KAMATI YA BUNGE YATEMBELEA MRADI WA UJEZI WA OFISI ZA TSC, YATOA MAELEKEZO



Wajumbe wa kamati ya Bunge ya Kudumu ya TAMISEMI wakikagua mradi wa ujenzi wa Jengo la Ofisi za TSC Makao Makuu jijini Dodoma tarehe 5 Novemba, 2024.

TSC MBIONI KUKAMILISHA MWONGOZO WA MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WAPYA KAZINI



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akifungua kikao kazi cha siku mbili kilichowahusisha wadau mbalimbali wa elimu kwa lengo kupitia rasimu ya mwongozo wa mafunzo elekezi kwa walimu wanaojiririwa kwenye Utumishi wa Umma, tarehe 21 Novemba, 2024 mjini Morogoro.

Na Mwandishi Wetu, TSC – Morogoro.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iliendesha kikao kazi cha kupitia rasimu ya Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaojiririwa kwenye Utumishi wa Umma ili waweze kuzingatia masuala muhimu yanayohusu Utumishi wao.

Akifungua kikao kazi hicho kinachoendeshwa na TSC kupitia Mradi wa Global Partnership for Education (GPE) tarehe 21 Novemba, 2024 mjini Morogoro, Mwenyekiti wa Tume Prof. Masoud Hadi Muruke alisema kuwa maboresho ya mwongozo huo ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya utumishi wa walimu nchini.

Alisisitiza kuwa mwongozo huo umeandaliwa ili kuondoa utofauti katika kuwaelekeza walimu wapya mara wanapojiririwa kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za

utumishi wa umma.

“Mwongozo umetoa maelekezo mahsusi kwa Walimu wapya kuhusu Misingi ya Utumishi wa Umma na Utumishi wa Walimu, haki na wajibu wao pamoja na miiko na maadili katika utekelezaji wa majukumu yao pamoja na taratibu zingine,” alisema.

Kwa upande wa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama alisema

kuwa mwongozo utawasaidia walimu wanaojiririwa katika Utumishi wa Umma Tanzania bara kupata uelewa mzuri wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia Utumishi wa Umma kwa ujumla na hususani katika Utumishi wa Walimu.

Mwl. Paulina aliongeza walimu wataweza kufahamu haki, wajibu, maadili yanayoongoza Utumishi wa Umma na taaluma ya kada yao kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi na hivyo kuwa na Utumishi wa Umma wenye tija na utoaji wa huduma bora kwa wateja.

Sanjari na hilo, Mwongozo huo unalenga kuwapatia walimu wapya taarifa za msingi kuhusu haki na wajibu wao kama watumishi wa umma, kuwawezesha kufahamu mbinu bora za kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kuwasisitiza umuhimu wa kujitambua kama watumishi wanaowajibika kwa jamii.

Aidha, Mwl. Paulina alisema kuwa mwongozo unalenga kuwaelimisha walimu kuhusu taratibu za kupanda madaraja, taratibu na hatua mbalimbali za kinidhamu, na umuhimu wa kudumisha uadilifu katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa neno la utangulizi wakati wa kufungua kikao kazi cha siku mbili kilichowahusisha wadau mbalimbali wa elimu kwa lengo kupitia rasimu ya mwongozo wa mafunzo elekezi kwa walimu wanaojiririwa kwenye Utumishi wa Umma, tarehe 21 Novemba, 2024 mjini Morogoro.

TSC MBIONI KUKAMILISHA MWONGOZO WA MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WAPYA KAZINI



Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mw. Fatuma Muya akiwasilisha mada juu ya rasimu ya mwongozo wa mafunzo elekezi kwa walimu wanaojirirwa kwenye Utumishi wa Umma kwenye kikao kazi cha wadau wa elimu tarehe 21 Nivemba, 2024 mjini Morogoro.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa kikao kazi cha kupitia rasimu ya mwongozo wa mafunzo elekezi kwa walimu wanaojirirwa kwenye Utumishi wa Umma tarehe 21 Novemba, 2024 mjini Morogoro.



Washiriki wa kikao kazi cha kupitia rasimu ya mwongozo wa mafunzo elekezi kwa walimu wanaojirirwa kwenye Utumishi wa Umma wakivaa kwenye ufunguzi wa kikao kazi hicho tarehe 21 Novemba, 2024 mjini Morogoro.

TSC MBIONI KUKAMILISHA MWONGOZO WA MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WAPYA KAZINI



WALIMU 1,120 WILAYANI KASULU WAMEPANDISHA VYEO KATIKA MWAKA 2023/24



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kasulu, Bw. Samwel S. Rubamba akitoa ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya ofisi hivi karibuni.

Na Mwandishi wetu – Kasulu.

Jumla ya Walimu 1,120 wa Shule za Msingi na Sekondari katika Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma wamepandishwa vyeo katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2023/24.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kasulu, Samwel S. Rubamba wakati wa mahojiano na Maafisa Habari wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TSC hivi Karibuni kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika ofisi hiyo.

Alisema kuwa kati ya walimu waliopandishwa vyeo kwa mwaka 2023/24 wa shule za Msingi walikuwa ni 813 na Shule za Sekondari ni 307 na kuongeza kuwa Walimu 132 walithibitishwa kazini ambapo Walimu wa Shule za Msingi ni 118 na Walimu wa Shule

za Sekondari ni 32.

Bw. Rubamba alisema kuwa katika kipindi hicho, jumla ya Walimu 53 walibadilishiwa muundo, kati ya hao Shule za Msingi ni 43 na Shule za Sekondari ni 10.

Akizungumzia suala la maadili na nidhamu kwa walimu, Bw. Rubamba alisema Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kasulu imeendelea kuwafikia walimu kwa lengo la kuwaelimisha umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na zile za Utumishi wa Umma ili kujiepusha na kukiuka maadili ya kazi hiyo.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kasulu inahudumia Halmashauri mbili ya Kasulu Mji na Wilaya ya Kasulu yenye jumla ya walimu 2,561 ambao Walimu wa shule za Msingi ni 1,923 na Walimu wa Shule za Sekondari ni 638.

Jukumu la kusimamia masuala ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya walimu lipo mikononi mwa Kamati ya TSC Wilaya, hiyo ni kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya Kasulu, Bw. Samwel S. Rubamba (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu Bw. Kazimoto M. Nkomoli (kulia) na Afisa Maadili na Nidhamu, Annastazia Saba (kushoto) hivi karibuni baada ya mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (HGU)



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akifunga kikao kazi cha siku mbili kilichowahusisha wadau mbalimbali wa elimu kwa lengo kupitia rasimu ya mwongozo wa mafunzo elekezi kwa walimu wanaoajiriwa kwenye Utumishi wa Umma, tarehe 22 Novemba, 2024 mjini Morogoro.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa neno la shukrani wakati wa kufunga kikao kazi cha siku mbili kilichowahusisha wadau mbalimbali wa elimu kwa lengo kupitia rasimu ya mwongozo wa mafunzo elekezi kwa walimu wanaoajiriwa kwenye Utumishi wa Umma, tarehe 22 Novemba, 2024 mjini Morogoro.



Washiriki wa kikao kazi cha kupitia rasimu ya mwongozo wa mafunzo elekezi kwa walimu wanaoajiriwa kwenye Utumishi wa Umma wakimsikiliza Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) (aliyesimama) wakati wa kufunga kikao kazi hicho tarehe 22 Novemba, 2024 mjini Morogoro.



Washiriki wa kikao kazi cha kupitia rasimu ya mwongozo wa mafunzo elekezi kwa walimu wanaoajiriwa kwenye Utumishi wa Umma wakati wa kufunga kikao kazi hicho tarehe 22 Novemba, 2024 mjini Morogoro.

WALIMU 567 BUHIGWE WAULA



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Buhigwe, Bw. Yusuph N. Ntibhinigira akitoa ufafanuzi kwa Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikali kuhusu utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo hivi karibuni.

Na Mwandishi wetu – Buhigwe.

Jumla ya Walimu 567 wa Shule za Msingi na Sekondari katika Wilaya ya Buhigwe mkoani Kigoma wamepandishwa vyeo katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2023/24.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Buhigwe, Bw. Yusuph N. Ntibhinigira wakati wa mahojiano na Maafisa Habari wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TSC hivi Karibuni kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika ofisi hiyo.

Alisema kuwa kati ya walimu waliopandishwa vyeo kwa mwaka 2023/24 wa shule za Msingi walikuwa ni 409 na Shule za Sekondari ni 158 na kuongeza kuwa Walimu 92 wa Halmashauri ya Buhigwe wamethibitishwa kazini ambapo Walimu wa Shule za Msingi ni 59 na Walimu wa Shule za Sekondari ni 33.

Bw. Ntibhinigira alisema kuwa katika kipindi hicho, jumla ya Walimu 17 walibadilishwa muundo ambapo

kati ya hao Shule za Msingi ni 15 na Shule za Sekondari ni 2.

Kwa upande wa maadili na nidhamu kwa walimu alisema Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Buhigwe imeendelea kuwafikia walimu kwa lengo la kuwaelimisha umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na zile za Utumishi wa Umma ili kujiepusha na kukiuka maadili ya kazi hiyo.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Buhigwe inahudumia walimu 1,094 ambao Walimu wa shule za Msingi ni 773 na Walimu wa Shule za Sekondari ni 321.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Buhigwe, Bw. Yusuph N. Ntibhinigira (kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu, Bw. Ignas Felix (kushoto) hivi karibuni baada ya mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.

TSC YAENDELEA KUJIIMARISHA KATIKA KUSHUGHULIKIA MASHAURI YA NIDHAMU NA RUFAA ZA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – TSC, Morogoro.

Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imejipanga kuimarisha utendaji kazi wake katika kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu wakati wa kushughulikia mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu ili kuendelea kutenda haki.

Hayo yameelezwa na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama tarehe 23 Novemba, 2024 wakati akifungua kikao kazi cha wataalamu wanaoandaa rasimu ya awali ya Mwongozo wa Mafunzo ya Usimamizi wa Masuala ya Nidhamu na Rufaa kwa walimu katika Utumishi wa Umma mjini Morogoro.

Mwl. Nkwama alisema Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imefanya jitihada mbalimbali katika kuimarisha Sekta ya Elimu jambo linalosaidia sekta hiyo kupiga hatua kimaendeleo ikiwa ni pamoja kuwezesha walimu kuwa na mazingira bora ya kazi na kuimarisha kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi.

Aliongeza kuwa ili kuhakikisha juhudi za Rais Samia zinaendelea kufanikiwa, katika eneo la ushughulikiaji wa mashauri ya nidhamu na rufaa kwa walimu, TSC haina budi kuimarisha mamlaka zake zote zinazotoa haki kuanzia ngazi ya shule, TSC Wilaya na TSC Makao Makuu.

Alisema mwongozo huo utatumika katika kutoa mafunzo kwa wahusika wanashughulika katika kila hatua ya kushughulikia mashauri ya nidhamu na Rufaa za walimu waliopo katika ngazi mbalimbali ndani ya Tume hiyo.

“Malengo yetu ni kuwa Mwongozo huu utakapokamilika makundi yote yanayohuka katika kutoa haki kwa walimu wakiwemo watumishi wote wa Tume lazima wapate mafunzo ya kutosha ili kuongeza uelewa wa masuala haya ya kisheria. Tunaamini kuwa



Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Fatuma Muya akitoa neno la utangulizi wakati wa kufungua kikao kazi cha wataalamu wanaoandaa rasimu ya awali ya Mwongozo wa Mafunzo ya Usimamizi wa Masuala ya Nidhamu na Rufaa kwa walimu katika Utumishi wa Umma tarehe 23 Novemba, 2024 mjini Morogoro.



Washiriki wa kikao kazi cha wataalamu wanaoandaa rasimu ya awali ya Mwongozo wa Mafunzo ya Usimamizi wa Masuala ya Nidhamu na Rufaa kwa walimu katika Utumishi wa Umma wakiwa katika hali ya utulivu wakati wa ufunguzi wa kikao kazi hicho tarehe 23 Novemba, 2024 mjini Morogoro.

hatua hii itasaidia kuongeza ufanisi katika utendaji wa kazi,” alisema Mwl. Nkwama.

Pia, Mwl. Nkwama aliongeza kuwa ufahamu wa walimu katika masuala mbalimbali ikiwemo haki zao katika mwenendo mzima wa kushughulikia mashauri ya nidhamu umeongezeka jambo ambalo limewafanya wengi wao kukata rufaa pale wanapokuwa hawakuridhika na uamuzi uliotolewa na mamlaka yao ya nidhamu katika kushughulikia mashauri yao ya nidhamu.

“Kwa sasa wapo walimu wanaokwenda mahakamani kuomba mahakama kuu ifanye mapitio ya mwenendo wa shauri (Judicial review) kwa kuwa wanatambua vizuri ushughulikiwaji na upatikanaji wa haki zao,” alisema.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akifungua kikao kazi cha wataalamu wanaoandaa rasimu ya awali ya Mwongozo wa Mafunzo ya Usimamizi wa Masuala ya Nidhamu na Rufaa kwa Walimu katika Utumishi wa Umma tarehe 23 Novemba, 2024 mjini Morogoro.

TSC YAENDELEA KUJIIMARISHA KATIKA KUSHUGHULIKIA MASHAURI YA NIDHAMU NA RUFAA ZA WALIMU



Washiriki wa kikao kazi cha wataalamu wanaoandaa rasimu ya awali ya Mwongozo wa Mafunzo ya Usimamizi wa Masuala ya Nidhamu na Rufaa kwa walimu katika Utumishi wa Umma wakiwa katika hali ya utulivu wakati wa ufunguzi wa kikao kazi hicho tarehe 23 Novemba, 2024 mjini Morogoro.

IFAHAMU TSC KYERA NA JITIHADA ZAKE KATIKA KUSIMAMIA WALIMU



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kyerwa, Bi. Valentina C. Majembe.

Na Mwandishi Wetu – Kyerwa.

Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kyerwa ipo katika mji wa Rwenkorongo uliopo umbali wa kilometa 200 kutoka Makao Makuu ya Mkoa wa Kagera.

Ofisi hiyo ina jumla ya Shule za msingi za Serikali ni 108 na Shule za Sekondari 28 na jumla ya walimu 1583 ambapo kati ya hao walimu 1186 ni wa shule za na walimu 397 ni wa shule za sekondari.

Bi. Valentina C. Majembe ni Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kyerwa ambaye hivi karibuni alipata fursa ya kufanya mahojiano na jarida hili na kueleza mafanikio mbalimbali ya ofisi hiyo katika kutoa huduma kwa walimu.

Alieleza kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 walimu 108 walisajiliwa na kuthibitishwa kazini huku walimu 979 wikipandishwa vyeo ambapo katika idadi hiyo walimu 773 walikuwa wa shule za msingi na 206 walikuwa wa shule za sekondari.

“Walimu 31 walibadilishiwa vyeo baada ya kukidhi vigezo kwa mujibu wa taratibu ambapo walimu 29 walikuwa wa shule za msingi na wawili (2) walikuwa wa shule za Sekondari. Walimu watatu (3) wa shule za msingi walipewa vibali vya kustaafu,” alisema Kaimu Katibu Msaidizi huyo.

Akizungumzia hali ya nidhamu kwa walimu wilayani hapo alisema, “katika kipindi cha miaka 2 niliyohudumu nikiwa Wilaya ya Kyerwa hali ya nidhamu kwa walimu ni nzuri kiasi, elimu zaidi inatakiwa kwa walimu ili kuepuka kutenda makosa kwa makusudi au kwa kutokujua taratibu za utumishi wa Umma.”

Kwa mujibu wa Bi. Majembe changamoto zinazowakabili walimu na kusababisha kukiuka maadili ya kazi yao ni pamoja na; uoro, ulevi, mikopo iliyopitiliza kwenye taasisi binafsi na kutokuwepo kwa mahusiano mazuri kati ya walimu wakuu na baadhi ya walimu wanaowaongoza.

Kiongozi huyo alihitimisha kwa kueleza kuwa elimu imeendelea kutolewa kwa wajumbe wa Kamati ya TSC wilayani hapo pamoja na wakuu wa shule ili kuimarisha utendajikazi wa Tume na kuwasaidia walimu kuzingatia sheria, kanuni na taratibu katika Maisha yao ya utumishi wa umma.

“Mafunzo ya wajumbe wa Kamati za Wilaya yanasaidia kuongeza ufanisi wa kujua sheria, kanuni na taratibu katika kuamua mashauri ya kinidhamu kwa walimu. Nashauri mafunzo hayo yawe yanafanyika kwa wajumbe wote ili kuendelea kuwa na uelewa wa pamoja katika kufanya maamuzi ya haki kwa walimu,” alisema.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kyerwa, Bi. Valentina C. Majembe (kushoto) akiwa katika picha ya pamopja na afisa wa TSC Kyerwa, Mwl Godwin T. John.

WALIMU 383 KAKONKO WAMEPANDISHWA VYEO KATIKA MWAKA WA FEDHA 2023/24



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kakonko, Bw. Kashirira E. Kashirira akitoa ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya ofisi hivi karibuni.

Na Mwandishi wetu – Kakonko.

Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kakonko mkoani Kigoma imepandisha Walimu 383 wa Shule za Msingi na Sekondari Wilaya hiyo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/24.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kakonko, Bw. Kashirira E. Kashirira wakati wa mahojiano na Maafisa Habari wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TSC hivi Karibuni kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika ofisi hiyo.

Alisema kuwa kati ya walimu waliopandishwa vyeo kwa mwaka 2023/24 wa shule za Msingi walikuwa ni 285 na Shule za Sekondari ni 98.

Bw. Kashirira alisema kuwa jumla ya Walimu 84 wa Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko walithibitishwa kazini ambao Walimu wa Shule za Msingi ni 68 na Walimu wa Shule za Sekondari ni 16.

Kutokana na mafanikio hayo, Kaimu Katibu Msaidizi huyo

limesaidia kuongeza kasi ya utendaji kazi shuleni na hivyo kuwezesha wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao.

“Rais Samia ameweka historia ya pekee katika wilaya yetu kwa kuhakikisha haki na maslahi ya walimu yanalindwa kwa nguvu zote. Tukiangalia mwaka 2023/24 tulipandisha vyeo walimu 383 hii ni hatua kubwa katika kuimarisha Sekta ya Elimu hapa nchini,” alisema.

Akizungumzia suala la maadili na nidhamu kwa walimu, Bw. Kashirira alisema Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kakonko imeendelea kuwafikia walimu kwa lengo la kuwaelimisha umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na zile za Utumishi wa Umma ili kujiepusha na kukiuka maadili ya kazi hiyo.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kakonko inahudumia jumla ya walimu 743 ambapo Walimu wa shule za Msingi ni 561 na Walimu wa Shule za Sekondari ni 182.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kakonko, Bw. Kashirira E. Kashirira (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC Kakonko, Bw. Jobson Rulihose (kushoto) na Afisa Maadili na Nidhamu, Bi. Chrisencia Nzenda (kulia).



Kikao cha Kamati ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ya Utarwala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma kikiwa kinaendelea katika ofisi za TSC Makao Makuu Dodoma tarehe 24 Novemba, 2024.

SERIKALI YAWASHIKA MKONO WALIMU 1,658 WILAYANI KIGOMA



Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kigoma, Bw. Azimu Kahisha akitoa ufafanuzi kwa Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikali (HGCU) kuhusu utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo hivi karibuni.

Na Mwandishi wetu – Kigoma.

Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kigoma imewapandisha vyeo Walimu 1,658 wa Shule za Msingi na Sekondari wa wilaya hiyo katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2023/24.

Hayo yameelezwa na Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC Wilaya ya Kigoma, Bw. Azimu Kahisha kwa niaba ya Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kigoma Nathany Balanzize wakati wa mahojiano na Maafisa Habari wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TSC hivi Karibuni kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika ofisi hiyo.

Alisema kuwa kati ya walimu waliopandishwa vyeo kwa mwaka 2023/24 wa shule za Msingi walikuwa ni 1,196 na Shule za Sekondari ni 472 na kuongeza kuwa Walimu 102 wa Wilaya ya Kigoma wamethibitishwa kazini ambapo

Manispaa ya Kigoma ni mwalimu mmoja (01) na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ni Walimu 102.

Bw. Kahisha alisema kuwa katika kipindi hicho, jumla ya Walimu 12 walibadilishwa muundo ambapo walimu nane (8) ni wa Manispaa ya Kigoma na walimu wanne (4) ni wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma.

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu wilayani Kigoma aliishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hatua iliyochuklua za kulinda maslahi ya walimu, jambo ambalo limesaidia kuongeza kasi ya utendaji kazi shuleni na hivyo kuwezesha wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao.

“Rais Samia ameweka historia ya pekee katika wilaya yetu kwa kuhakikisha haki na maslahi ya walimu yanalindwa kwa nguvu zote. Tukiangalia mwaka 2023/24 tulipandisha vyeo walimu 1,668 hii ni hatua kubwa katika kuimarisha Sekta ya Elimu,” alisema.


Akizungumzia suala la maadili na nidhamu kwa walimu, Jeska alisema Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kigoma imeendelea kuwafikia walimu kwa lengo la kuwaelimisha umuhimu



Afisa Maadili na Nidhamu Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kigoma Bi. Veronica Mgozi akitoa ufafanuzi kwa Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikali hivi karibuni.

wa kuzingatia sheria, kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na zile za Utumishi wa Umma ili kujiepusha na kukiuka maadili ya kazi hiyo.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kigoma inahudumia walimu 1,668 katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji na Halmashauri ya Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma.



Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kigoma Bw. Azimu Kahisha (kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Afisa Maadili na Nidhamu, Bi. Veronica Mgozi (kushoto) hivi karibuni baada ya mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.



Washiriki wa kikao kazi cha kupitia rasimu ya Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaojiririwa kwenye Utumishi wa Umma kilichoendeshwa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kupitia Mradi wa Global Partnership for Education (GPE) tarehe 21 - 22 Novemba, 2024 wakiwa kwenye kazi za vikundi kupitia rasimu ya mwongozo huo.



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

Hongera *Taifa Stars*

Kufuzu
AFCON 2025



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

NEEMA YAWASHUKIA WALIMU 964 WILAYANI UVINZA



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Uvinza, Bi. Jeska Nguwila (kulia) akitoa ufafanuzi kwa Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya ofisi hivi hivi karibuni.

Na Mwandishi wetu – Uvinza.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Uvinza imewapandisha vyeo walimu 964 wa shule za msini na Sekondari katika Halmashauri ya Wilaya hiyo katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2023/24.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Uvinza Bi. Jeska Nguwila wakati wa mahojiano na Maafisa Habari wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TSC hivi Karibuni kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika ofisi hiyo.

Alisema kuwa kati ya walimu waliopandishwa vyeo kwa mwaka 2023/24 wa shule za Msingi walikuwa ni 806 na Shule za Sekondari ni 158 na kuongeza kuwa Walimu 189 wamethibitishwa kazini ambapo Walimu wa Shule za Msingi ni 144 na Walimu wa Shule za Sekondari ni 45.

Bi. Jeska alisema kuwa katika



Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Uvinza, Bi. Scola Wilson akitoa ufafanuzi kwa Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini hivi karibuni.

kipindi hicho, jumla ya Walimu 4 waliobadilishwa muundo katika kati ya hao Shule za Msingi ni 2 na Shule za Sekondari ni 2.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Uvinza, Bi. Jeska Nguwila (kulia) akiwa katika picha na pamoja na Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu, Bi. Scola Wilson (kushoto) hivi karibuni baada ya mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.

Bi Jeska aliishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hatua alizochukua za kulinda maslahi ya walimu, jambo ambalo limesaidia kuongeza kasi ya utendaji kazi shuleni na hivyo kuwezesha wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao.

Akizungumzia suala la maadili na nidhamu kwa walimu, kiongozi huyo alisema Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Uvinza imeendelea kuwafikia walimu kwa lengo la kuwaelimisha umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na zile za Utumishi wa Umma ili kujiepusha na kukiuka maadili ya kazi hiyo.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Uvinza inahudumia walimu 1,570 ambao Walimu wa shule za Msingi ni 1,259 na Walimu wa Shule za Sekondari ni 311.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama tarehe 15 Novemba, 2024 ameongoza mamia ya waombolezaji kwenye mazishi ya aliyekuwa mtumishi wa TSC, Marehem Ramadhan Abdallah Ngaegela. Mazishi hayo yamefanyika Mbagala Kizuiani Dar es Salaam.



Mwili wa aliyekuwa mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Marehem Ramadhan Ngaegela ukitolewa nyumbani kwake Ihumwa jijini Dodoma kwa ajili ya kusafirishwa kwenda Mbagala Kizuiani Dar es Salaam kwa ajili ya mazishi.



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

TANZIA



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) anasikitika kuwatangazia kifo cha Mtumishi wa TSC, Mwl. **Ramadhan Abdallah Ngaegela** kilichotokea tarehe 13/11/2024 katika Hospitali ya Kanda ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma alipokuwa akipatiwa matibabu.

Marehemu Ngaegela alikuwa ni Afisa anayeshughulikia masuala ya Ajira na Maendeleo ya Walimu. Mazishi yatafanyika Mbagala Kizuiani Dar es salaam. Taarifa za tarehe ya mazishi zitatolewa mara baada ya taratibu kukamilika.

"Inna lilah wa inna ilayhi raji'un."



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu



Katibu wa Tume ya utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akisoma wasifu wa Marehem Ramadhan Ngaegela muda mfupi kabla ya mazishi yaliyofanyika tarehe 15 Novemba 2024 Mbagala Kizuiani Dar es Salaam.



Mmoja wa wanafamilia wa Marehem Ramadhan Ngaegela akitoa shukrani za familia kwa Tume ya utumishi wa Walimu pamoja na waombolezaji wote walioshiriki msiba huo.



Waombolezaji wakiwa katika msiba wa marehem Ramadhan Ngaegela tarehe 15 Novemba 2024 Mbagala Kizuiani Dar es Salaam.



Waombolezaji wakiwa katika msiba wa marehem Ramadhan Ngaegela tarehe 15 Novemba 2024 Mbagala Kizuiani Dar es Salaam.

OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

Hongera *Taifa Stars*

Kufuzu
AFCON 2025



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu